**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA AFYA**
**BARAZA LA WATAALAM WA MAABARA**
**Tovuti: www.hlpc.go.tz**
Simu: 0734005777

# MALIPO YA MTIHANI WA USAJILI WA APRILI 2025

Ofisi ya Msajili Baraza la Wataalam wa Maabara inawataarifu wahitimu wote wa taaluma ya maabara ya afya kuwa dirisha la maombi ya mtihani wa usajili utakaofanyika mwezi Aprili 2025 litafungwa tarehe 15.03.2025 hivyo kila mhitimu aliyetumikia usajili wa awali kama inavyoelekezwa kwenye miongozo wanasisitizwa kufanya maombi na kulipia mapema.

Aidha, kila mhitimu aliye na vigezo vya kufanya mtihani ambaye ameshachagua kituo cha mtihani anasisitizwa **kulipia mapema kabla ya tarehe 16.03.2025,** atakayelipia baada ya hapo hataweza kupata namba ya mtihani na hataruhusiwa kufanya mtihani. Hivyo waombaji wote wafanye malipo kabla ya tarehe tajwa ili kuondoa usumbufu utakaoweza kujitokea.

Mwombaji atakayefanya malipo kwa wakati atapata namba ya mtihani kwenye akaunti yake ya mfumo wa ***hprs.moh.go.tz*** kabla ya tarehe 17.03.2025. Aidha, aliyelipia mtihani kipindi cha nyuma na hakufanya mtihani atatumia namba ya mtihani inayooenekana kwenye akaunti yake

Ratiba ya tarehe za mitihani itatolewa mapema baada ya dirisha kufungwa.

Ofisi ya Msajili inawatakiwa utekelezaji mwema

Imetolewa na
Ofisi ya Msajili
Baraza la Wataalam wa Maabara
12.03.2025

HEALTH LABORATORY PRACTITIONERS COUNCIL
12 MAR 2025
P.O.Box 743
DODOMA